# KIZIDUO

## HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI.

**MUHTASARI WA KIKAO CHA WAKUU WA IDARA KILICHOFANYIKA KATIKA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (W) TAREHE 04.03.2022.**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA:**

1. Bw. Wambura Sunday - Mwenyekiti
2. Bw. Nyora C. Elias - Kaimu Afisa Utumishi (W) Katibu
3. Bw. Aloyce F.Gitambo - Kaimu Afisa Usafishaji na mazingira (W)
4. Bw. Zadi F. Midas - Kaimu Mweka Hazina (W)
5. Bw. Simeon Waryuba - Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W)
6. Dr. Emiliana Donald - Mganga Mkuu (W)
7. Bw. Kassimu S. Mnangwa - Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (W)
8. Bw. Antony Guzuye - Kaimu Afisa Elimu Sekondari (W)
9. Bw. Emmanuel I. Mwita - Kaimu Afisa HABARI
10. Bw. Idrissa M. Mkangara - Katibu wa Mikutano
11. Bw. John L. Meitamei - Afisa Maliasili (W)
12. Bibi. Palitha Cleophace - Afisa Elimu Msingi (W)
13. Bw. Samson Mnaga - Afisa TEHAMA (W)
14. Bw. Meek Mirambo - Kaimu Afisa Mipango (W)
15. Adv. Veronica C. Lukanda - Mwanasheria (W)
16. Bw. Tino Sabuni - Afisa Usafirishaji (W)
17. Eng. Nembris O. Kivuyo - Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W)

**AGENDA ZA KIKAO**

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha Agenda
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 10/12/2021
4. Yatokanayo
5. Yatokanayo na kamati za Kudumu
    - Kamati ya Elimu Afya na Maji Tarehe 21/10/2021

- Kamati ya uchumi, Ujenzi na Mazingira ya 22/10/2021
- Kamati ya kudhibiti Ukimwi ya Wilaya tarehe 18/10/2021
- Kamati ya fedha,Uongozi na Mipango ya tarehe 17/12/2021
- Taarifa ya changamoto za Kata (zilizotokana na kikao cha Baraza la madiwani kujadili taarifa za kata 4/11/2021)

6. Taarifa za utekelezaji kwa kipindi cha Robo ya Pili Oktoba hadi Desemba 2021 kwa idara zifuatazo.
    - Elimu Msingi, Elimu Sekondari na Afya
    - Idara ya Kilimo,Ushirika na Umwagiliaji, Mifugo na Uvuvi,Usafishaji na Mazingira, Maendeleo ya Jamii, Maliasili
    - Sekta ya Kudhibiti UKimwi
7. Taarifa ya mapato na matumizi kwa kipindi cha Mwezi Julai 2021 hadi Desemba 2021 (taarifa ya nusu mwaka)
8. Taarifa ya Idara ya Utawala na Utumishi kwa kipindi cha Oktoba hadi Desemba 2021
9. Taarifa ya miradi ya maendeleo kwa kipindi cha Oktoba hadi Desemba 2021
10. Taarifa ya Kitengo cha manunuzi kwa kipindi cha Oktoba hadi Desemba 2021
11. Taarifa ya mkaguzi wa Ndani kwa kipindi cha Oktoba hadi Desemba 2021
12. Taarifa kitengo cha Sheria kwa kipindi cha Oktoba hadi Desemba 2021
13. Taarifa ya utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo kwa kuwekewa herein za kielektronic.
14. Kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Anwani za Makazi
15. Taarifa ya utekelezaji wa mradi wa COVID – 19 ya madarasa 119 na nyumba moja ya watumishi 3 in one.
16. Taarifa za Serikali
17. Kufunga kikao

**MUHT. KUMB. NA. 65/2022/2023-KUFUNGUA KIKAO.**

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe na kuwajulisha kuwa hicho ni kikao cha kawaida.

Mwenyekiti aliwataarifu wajumbe kwamba alihudhuria kikao cha Bodi ya Brabara kilichofanyika Mkoani tarehe 01.03.2022 na kikao cha Baraza la Ushauri la Mkoa (RCC) kilichofanyika tarehe 03.03.2022.

Mwenyekiti aliaeleza kwamba katika kikao cha Bodi ya Barabara, waliweza kukagua miradi ya Barabara inayotekelezwa na TANROAD na TARURA. Katika ukaguzi wa miradi ya Barabara inayotengenezwa na TANROAD ilionekakana kuwa Bora zaidi katika ufanisi ukilinganisha na ile inayotekelezwa na TARURA.

Katika kikao hicho cha Bodi ya Barabara ya Mkoa, ilionekana kuwa TARURA wana changamoto ya kutengewa bajeti kidogo hali ambayo inasababisha kutokamika miradi kwa ufasaha.

Mwenyekiti aliwaeleza wajumbe kuwa, katika kikao hicho kulitolewa maagizo kuwa waandikiwe Barua Watendaji wa Kata na Vijiji kushiriki katika kusimamia Miradi ya Barabara katika maeneo yao.

Katika kikao cha kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC), Mwenyekiti aliwaeleza wajumbe kuwa uwekwe msisitizo wa kusimamia Ukusanyaji wa Mapato, Mitihani ya Kidato cha Nne na Darasa la Saba.

Pia walipitisha mabadiriko ya jina la Mji wa Mugumu na kuitwa Serengeti.

Vile Vile ilisisitizwa kwamba watumishi kuacha tabia ya kukusanya fedha za serikali na kutozipeleka Benki na kuzitumia bila kufuata utaratibu.

Imesisitizwa kwamba kitendo hicho hakikubaliki na atakaye bainika atachukuliwa hatua za kinidhamu.

Mwenyekiti aliendelea kuelezea kuwa ilisisitizwa kuwa, ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo ya Afya na Elimu inasimamiwa na kuhakikisha na kuhakikisha inakamilika kwa umakini na kwa wakati uliokusudiwa.

Pia ulitolewa msisitizo wa kufanyika kwa vikao vya kisheria ikiwemo kikao cha Ushauri cha Wilaya (DCC) na Mabaraza ya Biashara.

Mwenyekiti alielezea kuwa Mkuu wa Wilaya amekabidhiwa jukumu la kufuatilia vikundi vyote vilivyo pewa Mikopo ya Halmashauri na kujiridhisha kuwa hakuna vikundi hewa na taratibu zilizingatiwa.

Baada ya kusema hayo, alifungua kikao mnamo saa 4.05 Asubuhi.

**MUHT.KUMB.NA.66/2022/2023-KUTHIBITISHA AGENDA.**

Katibu aliwasilisha agenda 15 ili ziweze kujadiliwa.

Baada ya kuwasilishwa agenda 15, zilongezeka agenda mbili ambazo ni:

1. Uwekezaji wa Gurumeti kwenye vijiji vya Nyichoka, Park Nyigoti na Nyanungu.
2. Taarifa Ya Utekelezaji Wa Mpango Wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF III) Kwa Kipindi Cha Mwezi Oktoba Hadi Desemba 2021.

Wajumbe walipitisha na kulidhia agenda 18 zijadiliwe.

**MUHT.KUMB.NA.81/2022/2023 – TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA COVID -19 YA MADARASA 119 NA NYUMBA MOJA YA WATUMISHI 3 IN ONE.**

Taarifa iliwasilishwa na Idara ya Elimu Sekondari,Elimu Msingi na Mganga Mkuu (W).

Wajumbe walifahamishwa kuwa ujenzi wa Madarasa 119 yamekamilika kwa asilimia mia moja tayari yameanza kutumika.

Ujenzi wa nyumba moja ya watumishi watatu imekamilika ipo tayari kwa kutumika.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa ilipokelewa na wajumbe na kisha waliipitisha.

**MUHT.KUMB.NA.83/2022/2023- KUFUNGA KIKAO.**

Mhe. Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa uvumilivu kwa kumaliza kikao kwa wakati, alieleza kuwa ajenda zilikuwa nyingi na zilijadiliwa zote.

Baada ya kusema hayo alifunga kikao mnamo saa 9.47 Alasiri.

**MUHTASARI HUU UMETHIBITISHWA LEO TAREHE..............**

| | |
|---|---|
| **JINA.** DEOGRATIAS SAPI | **JINA.** Chatta Lueka |
| **SAINI.............................** | **SAINI.............................** |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI
S. L. P 176
MUGUMU / SERENGETI